

## MAPENZI YAMEGEUKA

*M.N.B. Mdumulla*

Shoto kulia kushoto, mapenzi yanaondoka  
Siyo mwendo wa kitoto, ila vumbi latimuka  
Hata ufungue mato, vigumu kuyamulika  
Utabaki unalia, dunia kugugumika!

Viumbe tumashakani, mapenzi kubadilika  
Ndani, juu na angani, ulimwengu unaruka  
Mashombo siyo ubani, mizoga imepasuka  
Maiti mia mamia, dunia imefurika!

Penzi limekuwa sumu, mapenzi yamegeuka  
Dharuba yake ni ngumu, ipigapo twaanguka  
Viongozi, mahakimu, hakuna kusalimika  
Madaraka wamevua, dunia imewashika!

Ukweli umepungua, mapenzi yamefutika  
Kejeli za kuchumia, hila na kuhadaika  
Mauti na kukamia, farakano na talaka  
Eti ndiyo masalia, dunia imegeuka!

Mabwana wamezuzuka, mapenzi kuyatapika  
Ndoa zinavyoanguka, kila siku zapasuka  
Kanuni wamezivuka, wake wasahaulika  
Wajibu wameuvua, dunia wakajivika!

Mkubwa hayuko kata! mapenzi yahasirika  
Kumbaki patapata, miseto na sokasoka  
Mapenzi yametupita, machoni kutufunika  
Mihemo imebakia, duniani yasikika.

Dunia sasa matata, mapenzi yakakasika  
Maovu yametupata, viungo vimevunjika  
Matumbo yakatakata, midomo kuachanika  
Tumepigwa na butaa, dunia kuachanika.

Urafiki unavia, mapenzi yanakatika  
Hakuna hata ulua, madhara yamelipuka  
Dunia ya kuonea, maguvu na madaraka  
Majoho yakunyonyea, dunia imepambika.

Ni risasi ya mauti, mapenzi yameshafika  
Akili hazidhatiti, mioyo imedhofika  
Yamenyauka matiti, na nyuso zimechafuka  
Hakuna lakumezea, dunia imekauka.

Urafiki wa maneno, mapenzi yakutamka  
Na kuumana kwa meno, makucha kukwaruzika  
Haupo hata unono, dhuluma imepandika  
Penzi limedidimia, dunia imebomoka.

Mabara yatafutana, mapenzi kuadimika  
Mizinga kwelekezana, udongo unachimbika  
Usalata na hiana, chokozi zinazalika  
Usawa unapotea, dunia yaaibika.

Mapenzi hasa ni nini, au sumu ya imani?  
Au wimbi la huzuni, yafanana na tufani?  
Au ndwele za moyoni, au donda akilini?  
Usaha inakojoa, dunia imevimbika.

Tafakari uyapime, mapenzi bila dhihaka  
Ubongo wako utume, ufike tulipofika  
Pumua kisha usome, chekecha kisha tamka  
Jaribu kuchungulia, dunia inavyowaka.

Kwa nini tukae hivi, mapenzi kutuvuruga?  
Vijana waota mvi, wazee kama wachanga!  
Twarushwa vile na vivi, kama mapumba na chenga!  
Tuchachamae yarudi, dunia iwe huria.

Jamia wenye fahamu, mnena kwa kuchora  
Aila zilo timamu, wahenga wenye busara  
Ketini mfanye hamu, mdurusi kwa ibara  
Mapenzi tuyarejeshe, imani dumu daima.